




Mfalme Chui  
aliendelea kuwa  
mzee.

Je, atamchagua  
mrithi wake namna  
gani?




Mfalme Chui  
aliwaita wanyama  
kwa sherehe.

Atawatangazia  
mpango wake.




Baada ya sherehe,  
Mfalme Chui  
alizungumza.

Wanyama  
walimsikiliza.




Alisema,  
"Mashindano  
yataamua  
atakayekuwa  
mfalme."



Atakayehesabu hadi  
kumi kabla ya mkuki  
kuanguka, atakuwa  
mfalme.




Tembo aliwasukuma  
wengine, "Mimi ni  
mkubwa. Ninastahili  
kuwa mfalme."




Tembo alihesabu  
hadi nne pekee.

Mkuki ulianguka.



Ngiri aliwasukuma  
wenzake akisema,  
"Nina nguvu zaidi.  
Nitakuwa mfalme."



Ngiri alihesabu hadi  
sita kisha mkuki  
ulianguka.

Aliondoka.



Wanyama walisema,  
"Tembo mkubwa na  
Ngiri wameshindwa.  
Nani atashinda?"



Sokwe alihesabu,  
"Moja! Mbili! Tatu!  
Nne! Tano! Sita!  
Saba!"

Alilia.




Mfalme Chui  
alisema, "Sokwe,  
unapate nafasi moja  
tu."

Sokwe aliondoka.



Baadhi ya wanyama  
walianza kuondoka.

Swara Mdogo  
alisema, "Hebu  
nijaribu."




Mfalme Chui  
aliwakemea, "Mpeni  
Swara nafasi.  
Mwache ajaribu."



Swara alisema,  
"Tano na tano ni  
kumi."

Mkuki ulianguka  
chini.



Mashindano  
yalionyesha  
mnyama mwerevu.

Swara alikuwa  
malkia baada ya  
chui.